**East African Journal of Swahili Studies**
eajss.eanso.org
**Volume 5, Issue 1, 2022**
**Print ISSN: 2707-3467 | Online ISSN: 2707-3475**
Title DOI: https://doi.org/10.37284/2707-3475

EAST AFRICAN NATURE & SCIENCE ORGANIZATION

*Original Article*

# Dhima ya Usimulizi Katika Uwasilishaji wa Nyimbo za Taarab: Uchunguzi wa Kipengele cha Wakati

*Dorcas Misoi[1], na Dkt. Richard Makhanu Wafula, PhD[1]*

[1] Chuo Kikuu cha Chuka, S. L. P. 109 - 60400, Chuka, Kenya.
[*] ORCID ID: https://orcid.org/0000-0002-8581-645X; Barua pepe ya mawasiliano: dorcasmisoi@gmail.com

**DOI ya Nakala: https://doi.org/10.37284/jammk.5.1.702**

**Tarehe ya Uchapishaji:**

*10 Juni 2022*

**Istilahi Muhimu**:

*Taarab, Mutribu, Naratolojia, Usimuliaji, Simulizi, Analepsia.*

**IKISIRI**

Taarab ni aina ya nyimbo yenye asili katika Pwani ya Afrika Mashariki. Nyimbo hizi kama zilivyo nyimbo zingine, ni zao la shughuli na hisia za binadamu. Hivyo, ujumbe katika nyimbo hizo hujikita katika miktadha mbalimbali ya jamii. Ntarangwi (2001) anasema, mbali na kuwa nyimbo za taarab huimbwa sana katika harusi za Waswahili, nyingi ya nyimbo hizo hugusia masuala mengine ya maisha kama vile uongozi, dini, urembo wa wanawake, mabadiliko ya kisiasa au hata kuhusu uchungu wa kumpoteza mpenzi. Masuala haya huwasilishwa na watribu kwa kutumia mbinu za lugha kwa ubunifu wa kiwango cha juu. Makala haya yamechunguza dhima ya usimulizi katika uwasilishaji wa nyimbo za taarab kwa kuzingatia kipengele mahsusi cha wakati. Kazi hii imeongozwa na nadharia ya naratolojia inayohusishwa na mwanafalsafa wa Kiyunani aitwaye Plato na kuendelezwa na wataalamu kama vile Genette, Stanzel, Manfred Jan na Mieke Bal. Nadharia hii inahusu usimuliaji wa hadithi. Misingi yake ni kuwa usimulizi lazima uwe na msimulizi, kitendo kinachosimuliwa, usemi kuhusu kinachofanyika, wahusika na dhamira ya usimulizi wowote hubainika kupitia kwa mtazamo wa msimulizi. Kipengele cha usimulizi cha wakati kimetumiwa kuonyesha dhima ya usimulizi katika uwasilishaji wa maudhui na mtindo wa uwasilishi katika nyimbo za taarab. Katika kufanya hivyo, makala haya yamebainisha kuwa kipengele cha usimulizi cha wakati kimedhihirika katika nyimbo teule za taarab na kimechangia kukuza maudhui na mtindo wa uwasilishi kwa kuonyesha kuwa wimbo wa taarab ni utanzu telezi unaosheheni usimulizi.

**APA CITATION**

Misoi, D., & Wafula, R. M. (2022). Dhima ya Usimulizi Katika Uwasilishaji wa Nyimbo za Taarab: Uchunguzi wa Kipengele cha Wakati. *East African Journal of Swahili Studies*, *5*(1), 161-170. https://doi.org/10.37284/jammk.5.1.702.

 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.5.1.702

**CHICAGO CITATION**

Misoi, Dorcas, & Richard Makhanu Wafula. 2022. "Dhima ya Usimulizi Katika Uwasilishaji wa Nyimbo za Taarab: Uchunguzi wa Kipengele cha Wakati". *East African Journal of Swahili Studies* 5 (1), 161-170. https://doi.org/10.37284/jammk.5.1.702.

**HARVARD CITATION**

Misoi, D. & Wafula, R. M. (2022) "Dhima ya Usimulizi Katika Uwasilishaji wa Nyimbo za Taarab: Uchunguzi wa Kipengele cha Wakati", *East African Journal of Swahili Studies*, 5(1), pp. 161-170. doi: 10.37284/jammk.5.1.702

**IEEE CITATION**

D. Misoi, & R. M. Wafula, "Dhima ya Usimulizi Katika Uwasilishaji wa Nyimbo za Taarab: Uchunguzi wa Kipengele cha Wakati", *EAJSS*, vol. 5, no. 1, pp. 161-170, Jun. 2022.

**MLA CITATION**

Misoi, Dorcas, & Richard Makhanu Wafula "Dhima ya Usimulizi Katika Uwasilishaji wa Nyimbo za Taarab: Uchunguzi wa Kipengele cha Wakati". *East African Journal of Swahili Studies*, Vol. 5, no. 1, Jun. 2022, pp. 161-170, doi:10.37284/jammk.5.1.702.

## UTANGULIZI

Kingei (2005) anasema kuwa, taarab ni nyimbo maarufu miongoni mwa Waswahili zenye sifa za kishairi zinazoambatana na ala za kimuziki zinazoimbwa katika hafla mbalimbali za kijamii. Anaongeza kuwa, neno taarab ni la asili ya lugha ya Kiarabu linalomaanisha kufurahi, sherehe au kuimba. Kimsingi, nyimbo hizo zilikusudiwa kusikilizwa tu. Zilitungwa kwa kuzingatia lugha ya kishairi yenye maneno yaliyo na urari wa vina na mapigo ya kimuziki.

Akiongezea haya, Topp (2014) anasema kuwa asili ya nyimbo za taarab ni Afrika Mashariki. Sultan Seyyid Barghash katika mwaka wa 1870, alimtuma Mohammed bin Ibrahim kwenda Misri kujifunza nyimbo za taarab ili aje amwimbie katika kasri lake. Aliporudi aliwafunza wanamuziki wengine waliomwimbia Sultan katika bendi iliyoitwa Ikwani Safaa. Katika mwaka wa 1911, Siti binti Saad kutoka katika kijiji cha Fumba alijiunga na bendi hiyo. Mbali na kuimba katika bendi hiyo, aliziimba nyimbo hizo katika hafla mbalimbali kwa lugha ya Kiswahili na Kiarabu na kuchangia katika kuenea kwa taarab katika mji wa Zanzibar na maeneo mengi ya Afrika Mashariki, Misri na Bombay. Nyimbo alizotunga ziliangazia matukio ya maisha ya kila siku.

Katika chapisho lake, Genette (1972) anashikilia kuwa, usimulizi ni maelezo ya mfuatano wa matukio ya kweli au ya kubuni kwa njia ya mdomo au kwa kuandikwa. Kulingana na Rimmon - Kenan (1983), usimulizi unahusu mambo matatu ambayo ni hadithi, usimuliaji na simulizi. Anasema, hadithi ni masimulizi ya matukio jinsi yalivyotokea kiwakati, usimuliaji ni kitendo cha kusimulia hadithi na simulizi ni matamshi au maandishi kuhusu tukio lililotendeka. Usimulizi unaweza kudhihirika katika nyimbo kwa kuwa kuna tukio au matukio yanayoelezwa kwa kuimbwa. Kuna mwimbaji na kauli kuhusu tukio au matukio yanayorejelewa. Usimulizi katika nyimbo za taarab huhusu masuala mbalimbali katika jamii kama vile uchumi, siasa, maadili, dini na mahusiano katika jamii. Makala haya yamechunguza uwepo wa kipengele cha usimulizi cha wakati katika nyimbo teule za taarab na hivyo kufanya nyimbo hizo kuwa simulio. Pia, yameonyesha nafasi ya kipengele hicho katika kukuza maudhui na mbinu za kimtindo na jinsi kupitia kwa usimulizi uliomo katika nyimbo hizo, wanajamii wanaweza kupata ujumbe unaokusudiwa.

## TAFITI KUHUSU USIMULIZI

Suala la usimulizi lilishughulikiwa na Ong'ondi (2005) kwenye riwaya ya *Walenisi*. Alichunguza vipengele vya usimulizi vya msimulizi wa hadithi, mtazamo, mpangilio wa hadithi, wakati na fikira na unenaji kwa kuzingatia mawazo ya Genette (1972). Alionyesha kuwa, mitazamo tofauti ilitumiwa kusimulia matukio tofauti na kuwa sehemu kubwa ya riwaya ilisimuliwa kwa mtazamo wa nje. Pia alionyesha mbinu nne za unenaji na fikira. Alidhihirisha uwepo wa usemi halisi, usemi wa taarifa, mfumo ulio wazi kuliko usemi halisi na mfumo ulio funge kuliko usemi wa taarifa katika riwaya hiyo.

Utafiti wa Arege (2012), ulishughulikia usimulizi katika *Utenzi wa Rasi'l Ghuli* kwa kuongozwa na nadharia ya naratolojia. Alichunguza vipengele vya

This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.5.1.702

wakati, daraja na sauti za usimulizi na wahusika. Uchunguzi wake ulidhihirisha kuwa utenzi huo ulitumia analepsia na prolepsia kwa wingi. Pia aligundua kuwa matukio mengi yaliwasilishwa kwa kurudiwarudiwa. Alidhihirisha uwepo wa daraja tatu za usimulizi na sauti ya kwanza, pili na tatu za usimulizi.

Kisurulia (2012), alitafiti kuhusu matumizi ya aina za mitazamo katika riwaya za Kiswahili kwa kutumia nadharia ya naratolojia. Aliangazia mtazamo ndani na mtazamo nje. Alibaini kuwa mitazamo ilitumika katika riwaya alizofanyia utafiti kwa njia tofauti. Kuna riwaya zilizotumia aina za mitazamo zaidi ya moja ilhali zingine zilitumia aina moja ya mtazamo. Mtazamo wa nje ulitumiwa zaidi kuliko mtazamo wa ndani. Vile vile, aligundua kuwa mbali na kuwa mitazamo huonyesha nia ya mwandishi, pia huathiri jinsi maana inayokusudiwa huwekwa wazi katika riwaya hizo.

Uchunguzi kuhusu usimulizi katika tamthilia ya *Kijiba cha Moyo na Mstahiki Meya* uliofanywa na Khamis (2015), ulinuia kubainisha vipengele vya usimulizi na dhima ya vipengele hivyo katika usimulizi wa hadithi kwenye tamthilia hizo. Alichunguza kipengele cha wakati, daraja na sauti za usimulizi na wahusika na uhusika. Utafiti wake ulibaini kuwa vipengele vya usimulizi vilikuwemo katika tamthilia hizo mbili na vilikuwa na umuhimu mkubwa katika kusimulia hadithi na kupitisha maudhui na dhamira za kazi hizo.

Naye Gathogo (2017), aliangazia mchango wa msimilishaji simulizi katika maonyesho ya filamu kwa kutumia nadharia ya naratolojia. Alinuia kutathmini namna msimilishaji simulizi anavyochangia maudhui katika lugha ya Kiswahili kwa kumrejelea D.J. Afro kama msimuliaji. Alibaini kuwa msimilishaji simulizi hutazama filamu asilia kwa kina ili kuufahamu ujumbe kisha baadaye kwa kutumia lugha ya Kiswahili husimulia filamu hiyo kwa kutumia ubunifu wake kuwasilisha maudhui ya filamu. Pia aligundua kuwa msimilishaji simulizi hujitungia visa vyake mbalimbali vinavyohusiana na tukio la uvamizi kwa lengo la kurahisisha uelewa wa filamu. Pia alibaini kuwa usimuliaji wa D.J. Afro ni msuko wa mbinu mbalimbali za lugha zinazofanikisha utazamaji wa filamu.

## TAFITI KUHUSU NYIMBO ZA TAARAB

Utafiti wa King'ei (1992), ulichunguza mchango wa nyimbo za taarab katika lugha, utamaduni na mawasiliano katika jamii kati ya miaka ya 1963–1990. Alijadili kuhusu mazingira ya kijiografia na ya kihistoria ya nyimbo za taarab, asili na maendeleo ya taarab, mtindo na maudhui katika nyimbo za taarab. Baadhi ya maudhui aliyoangazia katika nyimbo hizi yalikuwa maudhui ya siasa, utamaduni na ya kijamii. Alijadili kuhusu asili na historia ya taarab ya Afrika Mashariki na kusema kuwa taarab ya Afrika Mashariki ilianzishwa na makundi ya muziki yaliyoundwa na Sultani Seyyid Bargash aliyetawala kisiwa cha Unguja kati ya mwaka wa 1870 na 1888.

Utafiti kuhusu muziki, uana na dini kama vipengele vya utamaduni ambavyo huendelezwa katika maisha ya kila siku ya Waswahili wa Mombasa, Kenya ulifanywa na Ntarangwi (1998). Alizichunguza nyimbo za taarab na jinsi ambavyo nyimbo hizi hutumiwa kama chombo cha kusafirishia vipengele vya utamaduni vya dini na uana. Ntarangwi anasema kuwa 'taarab' ni neno la Kiswahili ambalo ni kisawe cha neno la kiarabu 'taarab', ambalo lamaanisha dhana ya kutumbuiza na kufurahisha. Ntarangwi anasema kuwa taarab ina upekee fulani ikilinganishwa na tanzu zingine za muziki wa Waswahili kwa kuwa ndiyo utanzu wa pekee ambao wanawake kwa wanaume hushirikiana katika kuimba na kucheza mbele ya hadhira.

Kea (2006), aliangazia suala la usemezo katika nyimbo za taarab. Alichunguza athari za muktadha na mazingira, uathiriano katika matini, uwepo wa matumizi ya sajili katika matini, ukanivali, malumbano na mtagusano wa nafsi katika matini. Aligundua kuwa sifa za usemezo katika nyimbo za taarab hujitokeza kwa njia tofauti katika nyimbo tofauti za taarab. Pia alibaini kuwa mazingira yalikuwa na nafasi kubwa katika utunzi na uimbaji wa nyimbo za taarab.

Uchunguzi kuhusu mwingiliano tanzu katika modern taarab – mipasho kwa kutumia nadharia ya usemezano ulifanywa na Murimi (2016), ambaye aliangazia mwingiliano tanzu katika nyimbo za taarab, miktadha ya mwingiliano tanzu katika nyimbo za taarab na majukumu yanayotekelezwa na tanzu za fasihi simulizi katika nyimbo za taarab.

This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.5.1.702

Utafiti wake ulibainisha kuwa, tanzu mbalimbali za fasihi simulizi zimeingiliana sana katika miainisho yake hali ambayo ilijidhihirisha katika modern taarab – mipasho. Alibaini kuwa, hakuna utanzu unaoweza kujisimamia bila kuathiriwa na tanzu zingine. Pia alidhihirisha miktadha mbalimbali ya mwingiliano tanzu katika muziki wa modern taarab - mipasho na kuonyesha kuwa hakuna utanzu unaoweza kujisimamia bila kuathiriana na tanzu zingine.

Uchunguzi wa dhamira na fani katika nyimbo teule za taarab za Shakila Saidi Khamisi ulishughulikiwa na Rashid (2018). Utafiti wake ulihusu dhamira mbalimbali katika nyimbo za taarab na mbinu za kisanaa katika nyimbo hizo. Matokeo ya utafiti wake yalibainisha uwepo wa dhamira mbalimbali na mbinu za kisanaa. Utafiti wake ulionyesha kuwa aliyoyasema msanii Shakila katika nyimbo hizo yaliakisi maisha halisi ya wanajaamii.

Kutokana na tafiti hizi zilizofanywa ilikuwa wazi kuwa, hakuna utafiti wa kina na dhahiri ambao ulichunguza usimulizi katika nyimbo za taarab hivyo kulikuwa na haja ya kufanya utafiti huu ili kubainisha jinsi tanzu za usimulizi na nyimbo za taarab zinavyoingiliana.

## MBINU ZA UTAFITI

Utafiti huu ulifanywa maktabani. Vitabu na makala mbalimbali kuhusu nadharia ya naratolojia yalipitiwa ili kupata matini ya nadharia na mihimili iliyoongoza uchanganuzi wa data. Vitabu vilivyoandikwa kuhusu historia na kusambaa kwa nyimbo za taarab vilisomwa. Tasnifu zilizoandikwa kuhusu usimulizi na nyimbo za taarab zilipitiwa. Data za kimsingi zilipatikana katika kanda za nyimbo teule za taarab zilizosikilizwa na kutazamwa kwa makini kisha beti zake kunakiliwa. Huduma ya mtandao ilitumika katika kupata habari muhimu kuhusu historia ya nyimbo za taarab na watribu wa nyimbo hizo. Data zilizokusanywa zilinukuliwa kwenye madaftari.

Baadhi ya nyimbo za taarab zilichunguzwa kwa kuzingatia lengo la utafiti. Mbinu ya usampulishaji ulikuwa wa kimaksudi. Misingi iliyotumika ilikuwa tajriba za watribu na nyimbo zenye ukwasi wa kipengele teule cha usimulizi na zilizotimiza lengo ya utafiti. Matokeo ya utafiti huu yaliwasilishwa kwa njia ya maandishi na yaliambatana na maelezo ya moja kwa moja kutoka kwa uchanganuzi wa data zilizopatikana. Maelezo yalihusu matokeo ya uchunguzi wa kipengele teule kilichofanyiwa utafiti, maudhui pamoja na mbinu za uwasilishi katika nyimbo teule za taarab kwa msingi wa nadharia ya naratolojia.

## NADHARIA YA NARATOLOJIA

Makala haya yaliongozwa na nadharia ya naratolojia. Nadharia hii inahusika na usimuliaji wa hadithi. Husaidia kuelewa, kuchanganua na kutathmini usimulizi. Prince (1982) anasema kuwa, suala kuu katika nadharia hii ni simulizi au usimulizi. Mwananaratolojia huchunguza kilichosimuliwa, matukio yaliyosimuliwa na usimulizi wenyewe na njia iliyotumiwa pamoja na ufanisi wake.

Nadharia hii iliwekewa msingi wa mawazo na mwanafalsafa wa Kiyunani Plato katika kitabu chake cha *The Republic* (1930). Alitoa maoni muhimu kuhusiana na usimuliaji ambao anaulinganisha na udhihirishaji. Plato anatumia dhana muhimu ya *daigesia* kwa maana *ya* uelezaji yaani msemaji anajitokeza waziwazi au anayetambulikana. Anatumia dhana ya *mimesia* kwa maana ya uonyeshaji au pale ambapo mtunzi hajitokezi waziwazi kama msemaji na huwa amefichika.

Genette katika *Narrative Discourse* (1972) alijadili nadharia ya naratolojia kwa kuzingatia misingi ya umuundo. Kipengele cha kwanza alichobainisha ni daraja tatu za usimulizi na sauti za msimulizi. Daraja hizo ni daraja ya kwanza (extradiegetic), ya pili (intradiegetic) na ya tatu (metadiegetic). Katika sauti za msimulizi kuna usimulizi wa nafsi ya kwanza (homodaigesia) na usimulizi wa nafsi ya tatu (heterodaigesia). Alizungumzia kipengele cha wakati katika hadithi. Kulingana naye, kuna wakati hadithi na wakati matini. Wakati Unahusu mpangilio, muda na idadi marudio. Mpangilio ni uhusiano kati ya wakati wa matukio katika hadithi na mpangilio wake katika usimulizi, muda ni uhusiano wa kiwakati katika hadithi nayo idadi marudio inahusu tukio limetokea mara ngapi katika hadithi. Kipengele kingine alichozungumzia Genette ni mtazamo. Kuna mtazamo wa ndani na mtazamo wa nje. Mtazamo ni mwelekeo au maoni

 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.5.1.702

kuhusu jambo fulani. Matukio katika hadithi huwasilishwa katika mwelekeo fulani. Pia alijadili mtindo wa usimulizi kuwa wa kimimesia na wa kidaijesia. Mtindo wa daijesia unajitokeza wakati ambapo msimulizi anaeleza matendo na kauli ya mhusika bila kuwaruhusu wazungumze. Katika mimesia, simulizi inawasilishwa kwa kuwasawiri wahusika katika mandhari fulani wakizungumza moja kwa moja.

Rimmon - Kenan (1983) anasema, wakati ni ule uhusiano wa jinsi matukio yamefuatana kati ya hadithi na matini. Ameainisha wakati kwa njia mbili, wakati matini na wakati hadithi. Wakati wa hadithi unahusu muda unaochukua hadithi kuanzia mwanzo hadi mwisho ilhali wakati matini ni muda anaochukua msomaji kusoma matini fulani. Wakati Unahusu muda, mpangilio na idadi marudio. Nyimbo za taarab zimetumia aina hizi za wakati katika kuwasilisha masuala mbalimbali za jamii.

## KIPENGELE CHA WAKATI NA DHIMA YAKE KATIKA UWASILISHAJI WA NYIMBO ZA TAARAB

Genette (1972) anasema kuwa, wakati wa usimulizi huwa hauambatani na mpangilio wa matukio kwenye hadithi, kuna wakati wa kutendeka kwa tukio linalosimuliwa na wakati wa kusimulia tukio hilo. Matukio mengine katika hadithi yanaweza kuwasilishwa kupitia kwa mbinu rejeshi (analepsia) na mengine kupitia kwa kisengere mbele (prolepsia). Anarejelea hali hii kwa dhana anakronia au mpangilio. Rimmon - Kenan (1983), anafafanua wakati kuwa ni uhusiano wa mfuatano wa matukio katika hadithi na matini. Ameainisha wakati katika aina tatu ambazo ni, mpangilio, idadi marudio na muda.

Mpangilio huonyesha iwapo tukio limetokea kama la kwanza, la pili, la mwisho, kabla au baadaye. Muda unahusu kipindi ambacho tukio limechukua kutendeka. Kwa mfano, muda wa saa moja, miaka miwili, muda mrefu, muda mfupi, kutoka mahali C hadi D. Idadi marudio huonyesha idadi ambayo tukio limetokea. Kwa mfano, kwa dakika moja, mwezi mmoja au kwenye ukurasa mmoja.

### Mpangilio

Mbinu rejeshi na kisengere mbele husababisha tofauti ya jinsi matukio hufuatana katika hadithi na matini. Genette (1972), anatumia dhana ya analepsia na prolepsia. Analepsia ni usimulizi wa matukio yaliyotendeka kabla ya yanayosimuliwa kwenye matini na prolepsia ni masimulizi ya matukio yatakayotendeka baada ya matukio yanayosimuliwa katika hadithi. Analepsia na prolepsia husukuma mbele masimulizi kwa kuegemeza hadithi nyingine kwenye hadithi inayosimuliwa. Analepsia huelezea yaliyotokea awali kuhusu mhusika anayesimuliwa, tukio fulani na kufafanua masimulizi yanayosimuliwa na yanayotokea wakati huo katika matini. Aina tatu za analepsia ni analepsia ya ndani, mseto na ya nje.

### Analepsia ya Ndani

Ni masimulizi kuhusu yaliyotendeka awali kabla ya yanayosimuliwa na kurejelewa kama mbinu rejeshi na kusimuliwa kwa mara ya kwanza baadaye kwenye matini badala ya wakati tendo lilipotokea. Analepsia hii inabainika katika wimbo wa *Utalijua Jiji*, msimulizi anamkashifu mke ambaye hakutimiza wajibu wake kama mke kwa mumewe kwa kusimulia mambo ambayo mke alimfanyia mumewe na kumsababisha mumewe kumuacha na kuoa mke mwingine. Mke aliyemchukua mume wa mwenzake anasimulia yale mke huyu alimfanyia mume wake katika ubeti wa kwanza.

*Kazi yako ufisadi, jeuri ngebe na nongwa*

*Karakana ya ukaidi, ukaani maembe gwagwa*

*Vituko vya makusudi, si bure we umerogwa*

*Badala ya soda baridi, ama juisi ya chungwa*

*Ushamba umekuzidi, andazi wanywea chogwa*

*Mwenzangu huna ujuzi, mpenzi umemuudhi*

*Kaja kwangu nimempokea*

Tukio lililotokea mwanzo katika masimulizi yanarejelewa baada ya mume kumwacha mke wake na kuoa mke mwingine. Msimulizi anasema kuwa mke huyo alimfanyia mume wake vituko kimakusudi, alikuwa jeuri na hakuwa na ujuzi wa kumuandalia mume wake vyakula. Msimulizi anaongeza kuwa yeye ndiye alimchukua mume wa mwenzake kwa kumfanyia mazuri hadi mume huyo akabaki kwake. Anasema;

This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.5.1.702

*Pokea chako kibomu, shoga nakutumia*

*Hata ukinilaumu, wako nishamchukua*

*Penzi ulimdhulumu, visa ukamfanyia*

*Chachandu vitamutamu, bwana hukumpatia*

*Bwana kapata wazimu, kashindwa kuvumilia*

*Kwangu akatia timu, tiba nikampatia*

Kupitia kwa analepsia hii maudhui ya kutowajibika kwa mke yanadhihirika. Katika ndoa kuna majukumu ya mume na mke. Mke anafaa kumuandalia mumewe vyakula vizuri ili kumridhisha. Ila mke hajawajibika anavyosema msimulizi kuwa mke hakumuandalia mume wake vyakula vitamu hali iliyomfanya mume kuhamia kwa msimulizi. Vile vile, maudhui ya usaliti yanabainika. Mume anamuacha mke wake na kumuoa mke mwingine baada ya mke wake kutomuandalia vyakula vyema badala ya kumrekebisha. Pia msimulizi anamsaliti shogake kwa kuchukua mume wake. Anasema kuwa hajali lawama zitakazotoka kwa shogake, yeye ashamchukua mume huyo na anampa mapenzi na vyakula vizuri. Mbali na hayo, maudhui ya ukatili yanadhihirika, msimulizi hana moyo wa huruma kwa shogake. Anamwambia kuwa hajali kuwa mumewe amemwacha shogake na kumuoa. Analepsia hii pia imekuza mbinu ya uwasilishi ya mbinu rejeshi. Masimulizi yote kuhusu vituko alivyofanya mke hadi akaachwa na mume wake yanawasilishwa kwa mbinu rejeshi.

**Analepsia Mseto**

Ni aina ya analepsia ambapo tukio lililotendeka kabla ya kuanza kwa masimulizi na kutokea baadaye katika masimulizi kisha linaunganika na masimulizi na kuendelea hata baada ya masimulizi hayo. Kwenye wimbo wa *Kujipamba Harusini*, mume analalamika kuwa mke wake hujipamba tu akienda kwenye harusi lakini akiwa nyumbani hajipambi. Haya yanatokea katika ubeti wa kwanza;

*Mume: Ni heri nisikufite, yanikerayo moyoni*

*Mke wangu siku zote, hujirembeshi kwa nini?*

*Hujipambi tuko sote, mpaka wende harusini?*

Tabia hii ya mke kujipamba akienda harusini na kutojipamba akiwa nyumbani imekuwa ikitendeka kwa muda na inaendelea hata wakati mume wake anasimulia kwa kuwa ni mazoea ya mke huyu. Jambo hili linamkera msimulizi na anaamua kulalamika. Katika ubeti wa tatu mume anasimulia kuwa amevumilia kuona jambo hilo kwa muda mrefu.

*Mume: Kukueleza siwati, ulosema hayatoshi*

*Siku nyingi tumeketi, moyo wanitononeshi*

*Wafurahisha umati, mimi hunifurahishi*

Analepsia hii inakuza maudhui ya utamaduni, mume anasimulia kuhusu mke wake ambaye hujipamba tu anapoenda harusini. Harusi ni mojawapo ya sherehe ya tamaduni za jamii ya Kiafrika. Watu wa jamii hii hufanya sherehe hii kila mara watu wanapooana. Mke huyu pia anaidhamini sherehe hii kwa kuwa nadhifu kila mara anapoihudhuria. Analepsia hii inakuza mbinu ya uwasilishi ya kisengere nyuma kwa kutujuza kuhusu mambo yaliyotendeka kabla ya masimulizi yanayosimuliwa.

**Analepsia ya Nje**

Hii ni analepsia kuhusu yaliyotokea kabla ya kuanza kwa masimulizi ya kwanza. Hii inadhihirika katika wimbo wa *Naona Uzito Moyo Wangu* kwenye ubeti wa tatu. Msimulizi anamwambia mpenzi wake walipokutana siku ya kwanza, alimwona kuwa mwanamke nadhifu na kumpenda kwa dhati. Msimulizi anasimulia yaliyotokea muda mrefu kabla ya masimulizi anayoyasimulia.

*Siku yetu moja, tulokutanika*

*Ghafla mbeja, niliswalitika*

*Nilivue koja, Ulilonivika*

Kupitia kwa analepsia hii maudhui ya mapenzi yanabainika. Msimulizi anakiri kuwa alipomwona msichana huyo nadhifu alijawa na mapenzi kwake. Pia analepsia hii inakuza mbinu ya uwasilishi ya mbinu rejeshi. Msimulizi anasimulia jinsi alikutana na mpenziwe.

Prolepsia zinapotumika katika masimulizi, huondoa taharuki inayojengeka katika masimulizi. Hueleza

This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

yatakayotendeka baadaye kwa mhusika anayesimuliwa na matukio au hadithi inayosimuliwa wakati huo katika matini. Prolepsia inayoangazia yatakayotokea baada ya masimulizi yanayosimuliwa kuisha inaitwa prolepsia ya nje.

Prolepsia inaweza kuhusu kipindi kabla ya masimulizi yanayosimuliwa kuisha lakini yatakayotokea baada ya yanayosimuliwa kwenye hiyo hadithi. Aina hii huitwa prolepsia ya ndani. Kwenye wimbo *Naona Uzito Moyo Wangu* katika kiitikio mshororo wa tatu, msimulizi anamwambia mpenziwe kuwa moyo wake hautaweza kustahimili hali ya kumkosa.

*Naona uzito, mwenzangu*

*Kuwa kama ndoto, pendo langu*

*Naona uzito, kukosa wewe hauwezi moyo wangu*

Prolepsia hii imedhihirika kwa kuwa, msimulizi anaishia kuteseka baadaye kabla ya masimulizi yake kuisha. Katika ubeti wa pili, msimulizi anasema kuwa anateseka kwa kumkosa mpenzi wake.

*lngawa sianzi, kwako muhibaka*

*Hili la mapenzi, nakupa hakika*

*Ukinza sikinzi, kwako nateseka*

Prolepsia hii inakuza maudhui ya mapenzi. Msimulizi anakiri kuwa haamini kuwa mpenziwe anataka kumuacha na itakuwa vigumu kuishi bila yeye. Anasema kuwa amekuwa na wapenzi wengi lakini alimpenda mpenzi huyu sana na ataathirika sana ikiwa atamkosa. Prolepsia hii imekuza mbinu ya uwasilishi ya kisengere mbele ambapo msimulizi ameeleza hali ambayo itampata baada ya kuachwa na mpenziwe.

Pia kuna prolepsia mseto ambayo hujumuisha prolepsia ya nje na prolepsia ya ndani. Husimulia kuhusu matukio ambayo yatatokea kabla ya masimulizi kuisha kisha kuendelea hata baada ya masimulizi hayo kuisha. Kwenye wimbo wa *Viumbe Wazito*, prolepsia hii inadhihirika katika kiitikio ambapo msimulizi anawaambia waja waliomtendea mabaya kuwa hatawawekea kinyongo bali atawatendea mema milele.

*Wema wangu haozi milele utabakia*

*Nifanyavyo roho radhi kinyongo sitowawekea*

*Fadhila mfadhili mbuzi binadamu ana maudhi kweli huyooo*

*Sivui ubinadamu kwa mliyonitendea*

Katika mshororo wa kumi na tatu msimulizi anasema kuwa hatajenga uadui nao kwa kuwa moyo wake umetulia na atawatendea wema kwa kuwa anajali utu. Hapa ni wazi kuwa tendo la msimulizi kuwatendea wema maadui wake limetokea kabla ya masimulizi kuisha, msimulizi anaposema anazidi kuwatendea wema maadui wake.

Prolepsia hii imekuza maudhui ya utu katika kiitikio cha wimbo huu ambapo msimulizi anasema kuwa kuna wakati aliwatendea wema waja na bado atawatendea wema hata baada ya waja hao kumsema vibaya. Pia inakuza maudhui ya usaliti kutoka kwa waja ambao walimtendea mabaya msimulizi baada ya kufanyiwa hisani. Waja hawa walitarajiwa kumshukuru msimulizi kwa kutendewa vyema badala yake walimsema vibaya kwa hivyo walimsaliti msimulizi. Kupitia kwa prolepsia hii mbinu ya uwasilishi ya kisengere mbele imekuzwa kwa kuwa msimulizi anatujuza kuwa ataendelea kuwatendea wema waja hao hata baada ya masimulizi haya.

**Muda**

Genette (1972) anasema kuwa, wakati wa hadithi huelezwa kwa kupima kipindi ambacho hadithi inayosimuliwa imechukua kama vile, dakika, saa, siku, miezi na hata miaka. Wakati wa matini huelezwa kwa kuangalia urefu wa matini kama vile idadi ya mistari na kurasa za matini.

Anapendekeza matumizi ya kasi katika kupima muda wa masimulizi. Kasi ni uhusiano usiobadilika wa muda unaochukua hadithi kusimuliwa na urefu wa matini. Kwa mfano, wakati wa mwaka mmoja katika maisha ya mhusika unachukuliwa kama ukurasa mmoja.

Rimmon - Kenan (1983), anaonyesha aina mbili za kasi ambazo ni muhtasari na mtuo. Muhtasari ni hali ambapo kiasi kidogo cha matini kinaeleza matukio mengi. Aina hii inabainika katika wimbo wa *Kujipamba Harusini* kwenye ubeti wa kwanza mshororo wa pili.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.5.1.702

*Mume: Ni heri nisikufite, yanikerayo moyoni*

*Mke wangu siku zote, hujirembeshi kwa nini?*

*Hujipambi tuko sote, mpaka wende harusini?*

Mume anasema mke wake siku zote hajirembeshi. Mume ametumia kiasi kidogo cha matini kueleza tukio lililotendeka siku nyingi. Hajataja siku hizo kwa majina amesema siku zote. Kupitia kwa muhtasari huu maudhui ya utamaduni unaohusu harusi yamebainika. Msimulizi anasema kuwa mke wake hujipamba anapoenda harusini tu, ina maana kwamba watu wa jamii hii wanathamini sana harusi na huandaa kila mara. Mbinu ya uwasilishi ya kisengere nyuma imekuzwa msimulizi anaposema siku zote. Anarejelea yaliyokuwa yakifanyika kabla ya masimulizi yanayosimuliwa. Katika ubeti wa tatu mshororo wa pili mume amesema siku nyingi huwa hana furaha.

*Mume: Kukueleza siwati, ulosema hayatoshi*

*Siku nyingi tumeketi, moyo wanitononeshi*

*Wafurahisha umati, mimi hunifurahishi*

Msimulizi ametumia neno siku nyingi badala ya kutaja kila siku kwa majina.

Mtuo ni hali ambapo sehemu kubwa ya matini inatoa maelezo kuhusu kipindi kifupi cha hadithi. Mtuo unaweza kuwa wa udondoshi au wa onyesho. Udondoshi ni kasi ya juu sana ambapo muda wa matini hausongi lakini muda wa hadithi unaendelea kwa kipindi fulani. Udondoshi unabainika katika kiitikio cha wimbo ambapo yale yanayosimuliwa yanarudiwa rudiwa. Hali hii inasababisha muda wa hadithi kuendelea ilhali muda wa matini hausongi. Mfano wa kiitikio ni katika wimbo wa *Naona Uzito Moyo Wangu* ambao ni:

Kiitikio;

*Naona uzito, mwenzangu*

*Kuwa kama ndoto, pendo langu*

*Naona uzito, kukosa wewe hauwezi moyo wangu*

Kiitikio hiki kinarudiwa baada ya kila ubeti. Kupitia kwa udondoshi huu maudhui ya mapenzi yamebainika. Msimulizi anamwambia mpenziwe kuwa haamini kuwa amemkataa na hataweza kuishi bila yeye.

Onyesho ni hali ambayo wakati hadithi na wakati matini ni sawa. Mfano wa onyesho ni katika dayalojia. Wimbo wa *Nguo Fupi* ni wa aina ya dayalojia kati ya baba na bintiye.

*Binti: Baba nakutaradhia, babangu nipa idhini*

*Kuna nguo zimeingia, mshono wa magotini*

*Wenzangu wajivalia, mimi sivai kwa nini?*

*Baba: Mwanangu haya ni yapi, wasema maneno gani?*

*Kivazi cha nguo fupi, si kivazi asilani*

*Ruhusa katu sikupi, heri upawe na nani*

Katika wimbo usimulizi unaohusu binti kumuomba babake ruhusa ya kuvaa nguo fupi na babake kukataa kumruhusu kwa kutoa sababu zake unakamilika wimbo unapoisha. Baba anakataa bintiye kuvaa nguo fupi kwa kuwa ni kujitoa thamani. Muda unaochukua usimulizi kukamilika ni sawa na muda ambao matini ya hadithi hiyo inachukua kukamilika. Kupitia kwa onyesho maudhui ya utamaduni kuhusu mavazi ya wanawake yamedhihirika. Kulingana na utamaduni wa jamii hii mwanamke anayeheshimika huvaa nguo ndefu. Vile vile maudhui ya ukengeushi yamebainika ambapo binti anataka kuacha kufuata utamaduni wake unaohusu mavazi yanayokubalika na kutaka kuiga mavazi ya utamaduni wa kigeni. Mbinu ya uwasilishi ya dayalojia imebainika kupitia kwa mazungumzo kati ya binti na babake.

### Idadi Marudio

Kulingana na Genette (1972), idadi marudio ni uhusiano kati ya idadi ambayo tukio limetokea katika hadithi na idadi ambayo tukio hilo limesimuliwa katika matini. Aina za idadi marudio ni usimulizi mosi, usimulizi rudufu na usimulizi banifu.

### Usimulizi Mosi

Ni aina ya usimulizi ambao tukio lilitokea mara moja linasimuliwa mara moja. Katika wimbo wa *Kujipamba Harusini* kwenye ubeti wa kwanza

This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.5.1.702

mume anamuuliza mkewe sababu ya kutojipamba akiwa nyumbani hadi aende harusini. Swali hili halijaulizwa tena kwenye wimbo mzima.

*Mume: Ni heri nisikufite, yanikerayo moyoni*

*Mke wangu siku zote, hujirembesha kwa nini?*

*Hujipambi tuko sote, mpaka wende harusini?*

Usimulizi huu umetokea mara moja tu katika wimbo huu. Aina hii ya usimulizi imeibua maudhui ya ndoa. Mume anaposema 'mke wangu' na kulalamika kuwa huwa hajipambi wanapokuwa pamoja.

**Usimulizi Rudufu**

Ni usimulizi ambao tukio lililotokea mara moja linasimuliwa zaidi ya mara moja. Kwenye wimbo wa *Nguo Fupi,* kiitikio chake kinasimulia jambo moja mara kadhaa kwa kiitikio hicho kurudiwarudiwa baada ya kila ubeti.

Kiitikio;

*Katu ruhusa sikupi, hila haliwezekani*

*Kuvalia nguo fupi, sikubali asilani*

Baba anasema kuwa hatampa bintiye ruhusa ya kuvaa nguo fupi. Anasimulia mara kwa mara msimamo wake baada ya kila ubeti. Usimulizi rudufu unasisitiza maudhui ya utamaduni wa jamii hii kuwa wanawake wanaoheshimika hawafai kuvaa nguo fupi. Pia inakuza mbinu ya kimtindo ya takriri ya kurudia maneno au kifungu cha maneno.

**Usimulizi Banifu**

Ni hali ya kusimulia mara moja tukio lililotokea mara nyingi. Katika wimbo wa *Umejuaje Kama Si Umbeya* katika ubeti wa kwanza, mshororo wa tano msimulizi Anakashifu kitendo cha mwenzake kutamani kila msichana mrembo apitaye. Jambo la kutamani wasichana warembo limetendeka mara nyingi ila limesimuliwa mara moja:

*Macho yako kama mamba, wala hujui kufumba, hakikupiti kitu kirembo*

Usimulizi huu unabainisha maudhui ya uasherati ambayo yanadhihirika kupitia kwa tabia ya mtu huyu anayetamani kila mwanamke mrembo.

## HITIMISHO

Makala haya yamedhihirisha uwepo wa kipengele cha usimulizi cha wakati katika nyimbo teule za taarab na kutathmini dhima ya kipengele hiki kwa kuongozwa na nadharia ya naratolojia. Kupitia kwa muda, mpangilio na idadi marudio, maudhui ya mapenzi, uasherati, utamaduni, ndoa, usaliti, ukatili na kutowajibika yamedhihirika. Aidha aina hizi za kipengele cha wakati kimekuza mbinu za uwasilishi za mbinu rejeshi, kisengere mbele na takriri. Ni wazi kuwa kipengele cha usimulizi ambacho huhusishwa na kazi za kinathari kama vile hadithi kimebainika katika nyimbo za taarab na kutekeleza majukumu kama kinavyofanya katika hadithi. Hivyo, nyimbo za taarab zinaweza kuchukuliwa kuwa simulio.

## MAREJELEO

Arege, T. (2012). Narration in Swahili Narrative Poetry: An Analysis of *Utenzi wa Rasi'l Ghuli.* Tasnifu ya uzamifu Chuo Kikuu cha Nairobi. (Haijachapishwa).

Gathogo, E. (2017). Mchango wa Msilimishaji katika Maonyesho ya Filamu: Mfano wa DJ. Afro. Tasnifu ya shahada ya uzamili Chuo Kikuu cha Kenyatta. (Haijachapishwa).

Genette, G. (1972). *Narrative Discourse*. Ithaca: Cornell University Press.

Kea, P. (2006). Usemezo Katika Nyimbo za Taarab. Tasnifu ya uzamili Chuo Kikuu cha Kenyatta. (Haijachapishwa).

Khamis, S. (2015). Uhakiki wa Usimulizi katika Tamthilia ya Kijiba Cha Moyo na Mstahiki Meya. Tasnifu ya shahada ya uzamili Chuo Kikuu.

King'ei, G. (1992). "Language, Culture and Communication: The Role of Swahili Taarab Songs in Kenya, 1963-1990". Unpublished Ph. D Dissertation, Howard University.

This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.5.1.702

King'ei, G. (2005). *Swahili Taarab: From Tradional Orality to a Globalized Art Form.*Lwati. (A Journal of Contemporary Research, Vol. 2, 2005, pp. 1-15): Kenyatta University, Nairobi.

Kisurulia, E.S. (2012). Point of View in the Kiswahili Novel: A Narratology Analysis of selected (Haijachapishwa).

Murimi, J. (2016). Mwingiliano Tanzu Katika Modern Taarabu – Mipasho. Tasnifu ya uzamifu Chuo Kikuu cha Moi. (Haijachapishwa).

Ntarangwi, M. (1998). Taarab Texts, Gender, and Islam in Urban East African Context: Social Transformations among the Waswahili of Mombasa, Kenya. Tasnifu ya uzamifu: University of Illinois at Urbana Champaign. (Haijachapishwa).

Ntarangwi (2001). A Social- historical and Contextual Analysis of Popular Musical Performance Among the Swahili of Mombasa Kenya. Nairobi: Cultural Analysis.

Plato (1930). *The Republic, Books 1 to 5 trans. P. Shorey*. Cambrigde: Havard University Press.

Ong'ondi, E. (2005). Usimulizi katika riwaya ya *Walenisi* ya Katama Mkangi. Tasnifu ya uzamili Chuo Kikuu cha Nairobi. (Haijachapishwa).

Prince, G. (1982). *Narratology*: *The Form and Functioning of Narrative*. Berlin: Mouton Publishers.

Rashid, A. (2018). Kuchunguza Dhamira na Fani katika Nyimbo za Taarab Asilia: Mifano ya nyimbo za Shakila Saidi Khamisi. Tasnifu ya uzamili Chuo Kikuu Huria cha Tanzania. (Haijachapishwa).

Rimmon – Kenan, S. (1983). *Narrative Fiction*. London: Methuen& Co. Ltd.

Topp, J. (2014). Taarab Music in Zanzibar in the Twentieth Century. London: Ashgate publishing.